4. **Isimu Jamii. (alama 10)**
(a) Kwa nini kulikuwa na haya ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. (alama 5)
Toa sababu **tano**.
(b) Eleza sifa **tano** za sajili ya magazeti. (alama 5)

**MTIHANI WA MWIGO WA CEKENAS – 2016**
**KISWAHILI**
**102/3**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**

**SEHEMU YA A**

**SWALI LA LAZIMA**

1. "Leo ndioyo mtanitambua. Mama gani anayemtazama mwana akigeuka afriti?"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Tambua 'mwana aliyegeuka afriti'na ueleze hulka zake nne. (alama 6)
   (c) Jadili maudhui yoyote matano yanayojitokeza katika hadithi husika. (alama 10)

**SEHEMU YA B**
**Mtahiki Meya; Timothy Arege**
**Jibu swali la 2 au 3.**

2. "Siku moja kabla ya kufika kwa wageni. Meya ana mkutano na wawakilishi wa wafanyikazi ambao wameketi mkabala naye".

   (a) Fafanua madai yaliyotolewa na wafanyakzi katiak mkutano huu. (alama 12)
   (b) Eleza jinsi Meya alivyojibu madai ya wawakilishi wa wafanyakazi. (alama 8)

3. Tamthlia ya mstahiki Meya ni kioo cha jamii ya nchi za Afrika zinazoendelea. Thibitisha. (alama 20)

**SEHEMU YA C**
**Kidagaa kimemwozea.**
**Jibu swali la 4 au 5.**

4. Elimu ya kajielewa sisi nani, na twatoka wapi, twaelekea wapi na utu tutaurejeshaje pahali pake....
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Taja mfano mmoja wa tamathali ya usemi kwenye dondoo. (alama 2)
   (c) Dhihirisha jinsi utu ulivyotoka pahali pake, ukiregelea riwaya nzima. (alama 14)

5. Thibitisha kauli kuwa, "Mla naye huliwa zamu yake ifukapo'. Ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

**SEHEMU YA D.**
**USHAIRI**
**Jibu swali la 6 au 7.**

6. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Angaza, mtazame mlimwengu
Bidii, nayo matokeo chungu
Wezesha, kuishi bila uchungu
        Teknolojia maendeleo.

Angaza, zitazame barabara
Aenda, kwa kasi pia salama
Bidhaa, sokoni upesi fika
        Teknolojia maendeleo.

Angaza, majokofu majumbani
Vyakula, na vinywaji hifadhika
Nafuu, zizima maji ridisha
        Teknolojia maendeleo.
Angaza, leo pote madukani
Mikebe, vyakula vinywaji tiwa

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Mimea, huwawirishwa haraka
Teknolojia maendeleo.

Angaza, nguo kwa mashine stimu
Upesi, runinga na simu juza
Angani, burudika eropleni
Teknolojia maendeleo.

Angaza, tarakilishi nguzoye
Mauzo, mawasiliano kwayo
tibani, ni mwenzi kwake tabibu
Teknolojia maendeleo.

Angaza, mja hajakoma katu
Shughuli, kila uchao shajara
Apate, tulia kwa ufanisi
Teknolojia maendeleo.

(a) Eleza dhamira ya msanii katika shairi hili. (alama 2)
(b) Onyesha mifano **mitano** ya maendeleo katika maisha ya binadamu. (alama 5)
(c) Eleza umbo la shairi hii. (alama 4)
(d) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. (alama 4)
(e) Eleza kwa kifupi mtazamo wa mshairi kuhusu teknolojia. (alama 3)
(f) (i) Majokofu
(ii) Hunawirisha
(iii) Shajara

7. **Soma shairi ifuatalo kish aujibu maswali.**

Jana ilikuwepo, ikapita
Kwenye giza la sahau
Jana ilipiga kuathiri
Athari ijayo leo
Leo tunajua kesho tunaibashiria

Kesho ipapo na hatuijui
Kesho, itapiga au itapuliza?
Au itapita pasi na chochote
Kama moshi usio mashiko?

Kesho hatuioni
Lakini yaja ...
Twaihisi
Twaihisi
Twaimaizi
Ipo,

Yajongea
Hiyo na taathira zake
Inakuja
Yasogea
Yaja mbio
Yafikia upeo unaoitwa leo
Basi kumbuka
Maisha ni ubishi, yakabili!
Maisha ni jasiri, jusurisha!
Maisha ni huzuni, yashinde!
Maisha ni msiba, uweze!

Maisha ni wajibu, tekeleza!
Maisha ni ni fumbo, liague!
Maisha ni tatizo, litatue!
Maisha ni ahadi, itemize!
Maisha mapambano, wana nayo!

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Maisha ni zawadi, ipokee!
Maisha ni mchezo, uxhezee!
Maisha ni nyimbo, iimbe!
Maisha ni fursa, itumie?
Maisha ni ureda, furahia!
Maisha maumbile, changamkie!
Maisha ni lengo, lifike!
Maisha ni mwendo, yaendee!
Maisha ni uzuri, ustarehee!
Maisha liwazo, yapumzikie!

(a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili. (alama 2)
(b) Fafanua maudhui ya shairi hili. (alama 6)
(c) Onyesha muundo wa shairi hili. (alama 4)
(d) Taja na ueleze tamathali tatu za semi alizotumia mwandishi wa shairi hili. (alama 6)
(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumia katika shairi. (alama 2)
Twaimaizi
Yajongea

**SEHEMU YA E**
**FASIHI SIMULIZI**
**Jibu swali la 8.**

8. (a) Misimu ni nini? (alama 2)
(b) Onyesha kwa kutoleo mifano minne, jinsi misimu huzuka. (alama 4)
(c) Eleza vikwazo vitano vya ukuaji wa Fasihi Simulizi. (alama 10)
(d) Tafautisha kati ya;
(i) Ngonjera za ushairi na za maigizo. (alama 2)
(ii) Ngoma na ngomezi. (alama 2)

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479